**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS IKULU**

***Dar es Salaam***
***14 Januari, 2025***

## TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amemtumia salamu za rambirambi Mkuu wa Mkoa wa Songwe Mhe. Daniel Godfrey Chongolo, kufuatia kifo cha aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Mbozi Mhe. Bi. Ester Alexander Mahawe.

Marehemu Mahawe amefariki leo tarehe 14 Januari, 2025 katika hospitali ya KCMC mkoani Kilimanjaro ambako alikuwa akipatiwa matibabu.

Rais Dkt. Samia anawapa pole familia, ndugu, jamaa na marafiki wa marehemu Mahawe.

Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu Mahawe mahala pema peponi, Amina.

Sharifa B. Nyanga
Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu